

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKINOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA MSINGI THEMI HILL
HOLIDAY PACKAGE APRIL 2020
KISWAHILI VII-

MUDA : SAA 11/2

JINA _____ DARASA _____ TAREHE _____

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A,B,C,D na E yenye maswali 45
2. Jibu maswali yote katika sehemu zote
3. Jibu maswali kwa kujaza jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi
4. Mwandiko uliowazi, nadhifu na unaosomeka bila shiada utakupatia alama halali

SEHEMU A : SARUFI

1. Konsonanti moja au mbili zinaungana na irabu au pengine konsonanti peke yake, huunda tamko moja linaloitwa _____
2. Irabu hutokana na herufi tano tu maarufu ambazo ni _____
3. Katika neno POLISI idadi ya silabi ni _____
4. Andika kama ni irabu, konsonanti, neno, silabi au sentensi

Mfano : soma ----- ni neno

K -----ni konsonanti

- (a) Mkoa ni
- (b) Baba analima ni
- (c) KO ni
- (d) U ni
- (e) P ni

5. Muunganiko wa silabi zaidi ya moja wenye kuleta maana hutwa _____
6. Maneno yaliyoambatana na kuleta maana kamili huitwa _____
7. Idadi ya maneno katika sentensi, Ndege wana sauti nzuri za kupendeza”ni _____
8. Katika maneno yafuatayo tenga silabi zake

Mfano: Wanacheza- silabi zake ni wa-na-che-za.

- (a) Mwanafunzi – silabi zake ni _____
- (b) Analima- silabi zake ni _____
- (c) Waimbaji – silabi zake ni _____
- (d) Amemwandikia – silabi zake ni _____

9. Maneno yafuatayo yamekosewa. Yaandike kwa usahihi,
Mfano : semanini _____ kwa usahihi ni themanini.
(a) Thamani kwa usahihi ni _____
(b) Garama kwa usahihi ni _____
(c) Zahabu kwa usahihi ni _____
(d) Sule kwa usahihi ni _____
(e) Thatha kwa usahihi ni _____

10. Katika sentensi zifuatazo, maneno yaliyopigiwa mstari yanamakosa. Tambua makosa hayo na kisha uziandike sentensi kwa maneno yaliyo sahihi.

Kwa mfano: kichwa cha habari kinasema, “wabadhirifu razima waazibiwe

Kwa usahihi: kichwa cha habari kinasema, “wabadirifu lazima waadhibiwe

(a) Kwani kira mtu ajui kitu cha kufanya.

(b) Husiwe mra rushwa, bari huwe mzarendo harisi

(c) Sijarizika na jinsi tunavyoshughulikia mazara ya UKIMWI

(d) Tulipopita magaribi ya kituo, gafla tuwakuta askali wa kutuliza gasia.

(e) Sungula na tembo walikalibishwa na ngedele kwenye kalamu.

11. Nakili sentensi kwa kutumia maneno yenye maana sawa na yaliyopigiwa mstari

Mfano: Kolowi alianza kuugua.

Jibu: Kolowi alianza kuumwa

(a) Kirundo akakata shauri kutafuta suluhisho.

.....

(b) Alifanya kazi kwa juhudi kubwa

.....

(c) Tatizo lilifikia tamati kutokana na juhudi yake.

.....

(d) Kidole kimoja hakivunji chawa.

.....

(e) Alipoingia ndani ya nyumba akaanza kuduwaa.

.....

12. Kamilisha methali zifuatazo.

(a) Majuto ni _____

(b) _____ si maungwana.

(c) _____ ndiye rafiki.

(d) Mdharau mwiba _____

(e) Lenye mwanzo _____

13. Katika swali hili umepewa methali tano. andika methali hizo kulingana na maelezo yanayofuata chini.

Methali

- (i) Akiba haienzi
- (ii) Umoja ni nguvu
- (iii) Damu ni nzito kuliko maji
- (iv) Haba na haba hujaza kibaba
- (v) Bandu bandu huisha gogo

- (a) Methali inayosisitiza umuhimu wa kuwathamini ndugu ni _____

- (b) Inaeleza umuhimu wa kushirikiana _____

- (c) Inasisitiza umuhimu wa kufanya juhudi katika kufanya jambo kwani hata kama jambo ni gumu, ukijitahidi utafanikiwa. _____

- (d) Inahimiza umuhimu wa kidunduliza na kutodharau kitu, hata kama ni kidogo

- (e) Inaelezea umuhimu wa kuweka akiba ili ikusaidie baadaye. _____

Soma kifungu cha habari kifuatacho na kisha ujibu maswali yanayofuata.

Wananchi wa mkundi wana miaka mingi ya shida ya maji. Kwao. Jua ni hasara zaidi ya unavyofikiri lakini mvua ni neema ya ajabu. Majira ya mvua watu wenye nyumba zenye mapaa makubwa na visima vikubwa huvuna maji mengi. Watu wasio na hifadhi ya kutosha ya maji majumbani, wao ni kila siku kuyasaka madimbwi. Bado wana matumaini kuwa ipo siku watasahau shida hiyo.

MASWALI

- 14. Hoja kuu katika habari hii ni _____
- 15. Wakazi wenye tatizo la maji katika habari hii ni _____
- 16. Watu wanaovuna maji mengi kwa mujibu wa habari hii ni _____
- 17. Andika maana ya maneno yaliyopigiwa mstari kwenye habari
 - (a) Majira ni _____
 - (b) Kiguu na njia _____
 - (c) Kuyasaka _____
- 18. Andika maana za nahau zifuatazo
 - (a) Mtu wa miraba minne _____
 - (b) Fua dafu _____
 - (c) Ona kijicho _____